JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

## TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU UTEUZI WA MADIWANI WANAWAKE WA VITI MAALUMU KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025

**Dodoma, 17 Novemba, 2025**

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 36(1)(d) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, kifungu cha 25(1)(c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 vikisomwa pamoja na kifungu cha 113 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake kilichofanyika tarehe 17 Novemba, 2025 imefanya uteuzi wa Madiwani Wanawake wa Viti Maalumu **1,385** kati ya Madiwani Wanawake wa Viti Maalumu **1,387** wanaopaswa kuwepo kwa mujibu wa Sheria.

Uteuzi wa nafasi mbili (02) za Madiwani Wanawake wa Viti Maalumu utafanyika baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa marudio katika kata za Mindu na Chamwino zilizopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Kata ya Mzinga iliyopo katika Halmshauri ya Manispaa ya Temeke ambapo uchaguzi uliahirishwa kutokana na vifo vya baadhi ya wagombea katika kata husika.

Katika uteuzi huo, vyama vya siasa vitano (05) vimefanikiwa kupata Madiwani Wanawake wa Viti Maalumu. Vyama hivyo ni: -

1. Chama cha Mapinduzi (CCM);
2. Chama cha Alliance for Change and Transparency (ACT – Wazalendo);
3. Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA);
4. Chama cha The Civic United Front (CUF – Chama cha Wananchi); na
5. Chama cha National Convention for Construction and Reform (NCCR – Mageuzi).

Orodha na idadi ya walioteuliwa kwa kila chama imetumwa kwa Makatibu wa Vyama vya Siasa husika na Wakurugenzi wa Halmashauri zote Tanzania Bara.

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**